

## MATUNZO YA SHAMBA NA UVUNAJI

Ili kupata mavuno yenye tija ni muhimu kutunza vizuri shamba la mizabibu. Matunzo ya shamba ni pamoja na kupalilia, kutifulia, kudhibiti visumbufu na kukatia mizabibu.

- Palilia shamba mara kwa mara ili kudhibiti magugu, kwa wastani palizi tatu zinatosha katika msimu mmoja .
- Ni muhumu kutifulia udongo kwenye shamba la mizabibu kila wakati ili kuvuna maji ya mvua.

## Udhibiti wa magonjwa na wadudu

Mzabibu ni mmea ambaio unashambuliwa sana na magonjwa na wadudu. Magonjwa makuu yanayoshambulia mizabibu ni Ubwiri vinyoya (Downy mildew) na Ubwiri unga (Powdery mildew).

## Jinsi ya Kuthibiti Ugonjwa wa Ubwiri vinyoya:

Kuna njia kuu mbili za kuthibiti ugonjwa huu:

### i). Kutumia kanuni bora za kilimo

- Choma moto mabaki ya mimea mara tu baada ya kukatia.
- Zingatia kuiwekea mizabibu viegemezo na kufungia matawi.
- Mimea inayoshabihiana na viini enezi kama vile nyanya, nyanya chungu, biringanya, viazi mviringo, pilipili hoho, bamia na mipapai isipandwe pamoja na mizabibu.
- Ndani au karibu na shamba la mizabibu.

- Zingatia usafi wa shamba wakati wote.

### ii) Kutumia viuatalifu

- Tumia viuatalifu vyenye kiambata amilifu cha Mancozeb mfano Dithane MZ 45 Kwa ajili ya kukingga
- Tumia viuatalifu vyenye viambata amilifu vya Mancozeb na Metalaxyl kama vile Ridomil, Masterkinga, Linkmil 72 WP kwa ajili ya kukingga na kutibu

NB: Tumia viuatalifu kulingana na maelekezo ya matumizi.

## Ugonjwa wa Ubwiri Unga:

Ugongwa huu hujitokeza sana kipindi cha kiangazi na huathiri mmea hasa sehemu za majani, matawi na matunda

## Jinsi ya Kudhibiti Ugonjwa huu:

### i). Kutumia kanuni bora za kilimo

- Choma moto mabaki ya mimea mara tu baada ya kukatia.
- Zingatia kuiwekea mizabibu viegemezo na kufungia matawi.
- Mimea inayoshabihiana na viini enezi kama vile nyanya, nyanya chungu, biringanya, viazi mviringo, pilipili hoho, bamia na mipapai isipandwe pamoja na mizabibu.
- Zingatia usafi wa shamba wakati wote.

### ii) Kutumia viuatalifu

- Tumia viuatalifu vyenye kiambata amilifu cha Hexaconazole kama vile Xanthol, Anvil na Innovex kwa ajili ya kukingga na kutibu.
- Dhibiti wadudu waharibifu kwa kutumia viuatalifu kama vile Selecron na Duduba

## Ukatiaji wa Mizabibu

Kukatia mizabibu ni kitendo cha kuondoa matawi kwenye mizabibu kwa lengo la kuupa mzabibu uwezo wa kuzaa matunda

## Jinsi ya kukatia Mizabibu

- Miche ya mizabibu iliyokuzwa na kufikia urefu wa sentimita 160 – 180 hukatwa juu ili kuuwezesha mmea kukomaa
- Baada ya miezi 9 hadi 10 mizabibu huwa imekomaa kwa ajili ya mkato wa kwanza
- Hesabu macho 3 hadi 4 yaliyo juu ya waya wa kwanza na acha urefu wa sentimita 2 juu ya jicho la mwisho, kisha kata tawi na funga kwa kamba.
- Macho yakishachipua na kutoa matawi, yafunge matawi hayo kwenye waya wa pili.
- Pogolea machipukizi yote yanayoota chini ya waya wa kwanza.
- Msimu unaofuata chagua tawi la mwisho ili uendelee kuurefusha mkono

(cordon) na wakati huohuo katia kwa kuacha macho 2 katika kila tawi.

- Kwa wastani mche mkubwa wenyewe afya bora huachiwa macho 25 hadi 35, na kama macho yakichipua huchipua kwa wastani wa asilimia 75.
- Wakati wa kiangazi au sehemu zilizo kame, unashauriwa kuuachia mzabibu macho machache kuliko wakati wa mvua



Mzabibu unavyoonekana baada ya kukatia

#### Faida za Kukatia Mizabibu

- Kuiwezesha mzabibu kuzaa vizuri
- Kuupa mzabibu uwezo wa kugawanya vizuri chakula hasa kwenye mikono na matawi ya uzazi
- Kurahisisha uhudumiaji
- Kuondoa matawi yaliyo dhaifu, na yaliyoshambuliwa na magonjwa na wadudu
- Kuondoa maficho ya wadudu waharibifu na vimelea vya magonjwa

#### Uvunaji wa Zabibu

Zabibu huwa tayari kuvunwa baada ya siku 100 hadi 150 tangu kukatia kutegemea na aina ya mzabibu. Zabibu ni lazima zivunwe zikiwa zimeiva katika mti wake. Njia rahisi ya kujuza kwamba zabibu zimeiva ni:-

- Kuonja:- Ladha ya utamu ni kiashiria cha kwamba zabibu zimeiva. Ladha ya uchachu ni kiashiria kwamba zabibu hazijaiva.
- Rangi:- Baadhi ya aina za zabibu hubadilika rangi zinapoiva japo njia hii hujumuishwa na njia ya kuonja
- Kutumia Kifaa maalum (Refractometer) kifaa hiki hutumika kupima kiwango cha sukari katika zabibu
- Zabibu zilizoiva huwa na kiwango cha sukari (Brix) 20 hadi 26

#### KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI),  
Kituo cha Makutupora,  
S.L.P 1676,  
Dodoma, Tanzania  
Simu: +255 26 2961994,  
Barua pepe: [cdmakutupora@tari.go.tz](mailto:cdmakutupora@tari.go.tz)

#### TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA



#### MATUNZO YA SHAMBA NA UVUNAJI WA ZABIBU

